HOTUBA YA MHE. ENG. EVARIST NDIKILO, MKUU WA MKOA WA PWANI KWENYE MKUTANO WA WADAU WA MUHOGO MKOA WA PWANI TAREHE 15 APRILI, 2021

- ***Dkt. Delphine D. Magere, Katibu Tawala Mkoa wa Pwani,***
- ***Wahe. Wakuu wa Wilaya za Mkoani wa Pwani,***
- ***Mhe. Mwantumu Mahiza, Mkuu wa Mkoa Mstaafu na Mwenyekiti wa TACAPPA Taifa,***
- ***Wah. Wenyeviti wa Halmashauri za Wilaya na Mji Mkoa wa Pwani,***
- ***Wakuu wa Sehemu na Vitengo wa Sekretarieti ya Mkoa,***
- ***Makatibu Tawala wa Wilaya za Mkoa wa Pwani,***
- ***Wakurugenzi wa Halmashauri Mkoa wa Pwani,***
- ***Makamu Mwenyekiti wa TCCIA - Kilimo Mkoa wa Pwani,***
- ***Mwakilishi wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo (TARI-Kibaha),***
- ***Mwakilishi wa Taasisi ya Udhibiti Ubora wa Mbegu (TOSCI),***
- ***Wawakilishi kutoka Mashirika yasiyo ya Kiserikali IITA na MEDA,***
- ***Maafisa wa Chama cha Wadau wa Zao la Muhogo (TACAPPA),***
- ***Mrajis Msaidizi wa Vyama vya Ushirika Mkoa wa Pwani,***
- ***Maafisa Kilimo Sekretarieti ya Mkoa,***
- ***Maafisa Kilimo, Ushirika na Umwagiliaji wa Halmashauri,***
- ***Wanunuzi wa zao la muhogo Mkoa wa Pwani,***
- ***Wamiliki wa Viwanda Vidogo vya kusindika zao la Muhogo,***
- ***Wazalishaji wa mbegu za Muhogo,***
- ***Wawakilishi wa Wakulima wa Muhogo Mkoani Pwani,***
- ***Waandishi wa Habari.***
- ***Mabibi na Mabwana.***

Ndugu Wadau;

Awali ya yote nitumie fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kukutana hapa tukiwa wazima na wenye afya njema.

Pili, nawashukuru waandaaji wa Mkutano huu chini ya usimamizi wa Katibu Tawala wa Mkoa; kwanza kwa kuona umuhimu wa kuwa na Mkutano huu muhimu kwa tasnia ya Muhogo ndani ya Mkoa wetu na pili, kwa kunipa fursa ya kuufungua na kushiriki.

Tatu, nawashukuru Umoja wa Wazalishaji na Wasindikaji wa Muhogo Nchini (Tanzania Cassava Producers na Processors - TACAPPA) kwa uamuzi wao wa kuutembelea Mkoa wa Pwani kwa lengo la kujitambulisha na pia kutuletea fursa muhimu sana kwenye tasnia ya Muhogo. Wakati muafaka utakapofika tutasikia kutoka kwao ambapo watatueleza fursa hizo na wajibu wetu kama Wadau ili tuweze kufikia matarajio.

Nitoe shukurani mahsusi kabisa kwa Mwenyekiti wa TACAPPA Mheshimiwa Mwantumu Mahiza, Mkuu wa Mkoa Mstaafu ambaye pia alihudumu kama Mkuu wa Mkoa wa Pwani aliyeniachia kijiti cha kuongoza Mkoa huu kwa uzalendo wake wa kukumbuka nyumbani. Mheshimiwa Mahiza alipokuwa hapa Mkoani alikuwa mstari wa mbele kusukuma tasnia ya Muhogo. Ni katika kipindi chake katika Mkutano wa Wadau kama huu ambapo lilitolewa azimio la kila kaya kulima angalau ekari mbili (2) za Muhogo, moja (1) kwa ajili ya chakula na nyingine kwa ajili ya biashara. Aidha, nimshukuru Mhe. Mercy Silla, ambaye alikuwa ni Mkuu wa Wilaya ya Mkuranga katika kipindi hicho na ambaye pia ni Mjumbe muhimu kwenye TACAPPA, kwanza kwa kusukuma uzalishaji wa Muhogo Wilayani

Mkuranga hadi leo Wilaya ile ina Uzalishaji mkubwa wa Muhogo, ina Wazalishaji wengi wa mbegu na pia ina Vikundi vingi vya Wasindikaji wa Muhogo. Kitendo cha Viongozi hawa Wastaafu kuukumbuka Mkoa waliofanyia kazi na kuamua kuja kukutana nasi Wadau ili kutuletea mambo mazuri kuhusiana na zao la Muhogo ni uzalendo wa hali ya juu unaopaswa kupongezwa na kila mmoja wetu.

Mwisho, kwa shukurani ingawa siyo kwa umuhimu, naomba niwashukuru na kuwakaribisha Wadau wote kushiriki kwenye Mkutano huu muhimu. Niombe ushiriki wenu wa dhati katika kujadili na kuchangia masuala mbalimbali yatakayowasilishwa mbele yetu, ili hatimaye tutoke na maazimio mazuri yenye tija na yanayotekelezeka kwa maslahi mapana ya Tasnia ya Muhogo.

Ndugu Wadau,

Zao la Muhogo ni zao kuu katika Mkoa wetu linalotuhakikishia usalama wa chakula na pia limeendelea kuwa chanzo cha fedha kwa wakulima.

Kwa upande wa fursa, zao hili lina fursa nyingi. Ni zao linalostawi kwenye Wilaya na Halmashauri zote likiwa na uwezo wa kustawi kwenye maeneo yenye mvua kidogo. Aidha, lina matumizi mengi kama kupika ukiwa mbichi, kusindika unga, kutengeneza wanga na chakula cha mifugo.

Ndugu Wadau,

Pamoja na umuhimu na fursa zinazotokana na zao hili, mtakubaliana nami kwamba halijachangia vilivyo kwenye uchumi wa Mkoa wetu.

Eneo linalolimwa zao la Muhogo ni dogo sana, wastani wa hekta **60,703** na kuzalisha tani **500,000** hadi **650,000** kwa mwaka. Eneo hili ni asilimia **3.1** ikilinganishwa na eneo linalofaa kwa kilimo, yaani hekta **1,933,224.** Mkoa wa Tanga majirani zetu ambao tupo kwenye Kanda moja yenye hali ya hewa na udongo unaofanana, wanalima wastani wa hekta 113,000 na kuzalisha wastani wa tani 850,000 hadi 1,000,000 kwa mwaka.

Kwa upande wa tija, nayo ipo chini. Kwa mfano, miaka mitano (5) iliyopita, uzalishaji kwa eneo ni wastani wa tani **6.5** hadi **7.6** kwa hekta ingawa yapo maeneo machache, hasa Wilaya za Kibiti na Rufiji ambako tija ni kati ya tani **9** hadi **18** kwa hekta. Tija inayopendekezwa kitaalam ni tani **20** kwa hekta.

Pamoja na kuwa chini kwa upande wa eneo, uzalishaji na tija, zao hili limekuwa ni la msaada mkubwa kwetu. Mkoa wa Pwani hatuna njaa. Wakulima wanapata fedha kwa kuuza Muhogo na kuendesha maisha yao, n.k. Kwa msingi huo, napenda kuwapongeza Wakulima wote, Watafiti, Maafisa ugani, Viongozi na Watendaji mbalimbali kwa kazi kubwa mnayofanya ya kuimarisha uzalishaji wa zao la Muhogo. Napenda kuwapa shime tuendeleze juhudi zaidi ili tuitumie fursa hii muhimu.

Ndugu Wadau,

Eneo lingine kuhusiana na zao la Muhogo ni usindikaji. Mkoa wetu hatufanyi vizuri pia katika eneo hili. Zimekuwepo juhudi mbalimbali za kuanzisha Vikundi na Viwanda vya Usindikaji. Matokeo ya jitihada hizi siyo ya kuridhisha. Vikundi karibu 32 vilivyoenea maeneo mengi ya mkoa wetu havisindiki Muhogo kwa madai kwamba wanakosa soko. Viwanda navyo havijatoa mchango uliokusudiwa kutokana na changamoto za uwekezaji na

uendeshaji. Kwa hiyo kwa ujumla, kiasi kikubwa cha Muhogo unaozalishwa Mkoani Pwani unaliwa ukiwa mbichi na mwingine kukaushwa kama makopa. Kiasi kidogo sana, tani 60 - 70 husindikwa kupitia Vikundi mbalimbali.

Pamoja na changamoto hizo, bado usindikaji ungekuwa eneo muafaka kwa ajili kusindika muhogo mwingi unaoharibika mashambani kutokana na kukosa soko. Nimeelezwa moja ya agenda ya leo ya TACAPPA ni kutueleza jinsi Mkoa wetu unavyoweza kushiriki kwenye suala zima la usindikaji wa Muhogo. Bila shaka kila mmoja wetu ana hamu kubwa kusikia TACAPPA watatuambia nini. Ombi langu kwetu sote ni kujipanga ili kukidhi mahitaji ya usindikaji huo.

Ndugu Wadau,

Huwezi kuzungumzia uzalishaji wa zao la Muhogo bila kutambua mchango wa Utafiti, Uzalishaji na Usambazaji wa Mbegu bora na Huduma za ugani (elimu kwa wakulima). Ukiachilia mbali eneo, kiwango cha uzalishaji na tija vinategemea sana aina ya mbegu zinazotumika na jinsi wakulima wanavyotumia utaalam katika kilimo chao. Tukitaka kutoka hapa tulipo ni lazima tuzingatie masuala ya utafiti wa mbegu bora zenye kuzaa sana, kuhimili magonjwa na wadudu na pia zinazotakiwa sokoni. Aidha, wakulima wetu wanatakiwa kufundishwa kanuni za kilimo bora ikiwamo kuandaa vema mashamba yao, kupanda kwa nafasi na kuzingatia kalenda za kilimo.

Napenda kutumia fursa hii kuwashukuru na kuwapongeza Watafiti wetu kupitia TARI Kibaha na Washirika wao TOSCI (Udhibiti wa ubora) na MEDA kwa Utafiti, Uzalishaji na Usambazaji wa mbegu bora zenye sifa.

Aidha, nawashukuru Maafisa ugani walioenea kote Mkoani kwa kazi kubwa ya kuwaelimisha wakulima.

Napenda kuwahimiza kuongeza bidii zaidi kila mmoja kwenye eneo lake ili tuongeze uzalishaji na tija zaidi.

Ndugu Wadau,

Tunapoelekea kuanza mkutano wetu, nawaomba Wadau wote tusikilize kwa umakini mada zote zitakazowasilishwa mbele yetu, kuzijadili na kuchangia mawazo ili tufikie maazimio yenye kutekelezeka. Lengo letu liwe kuboresha zao letu la Muhogo katika nyanja zote kama nilivyoeleza kwa kirefu hapo juu.

Ndugu Wadau,

Mwisho niwashukuru wote kwa mara nyingine kwa kuhudhuria mkutano huu muhimu wa aina yake kwenye sekta ya muhogo. Niwaombe tena tuchangie mada zote zitakazowasilishwa mbele yetu kwa uwazi na uhuru kwa lengo la kujenga tasnia yetu na Mkoa wetu.

Baada ya kusema hayo sasa natamka kwamba Mkutano wa Siku Moja wa Wadau wa Muhogo Mkoani Pwani Umefunguliwa rasmi.

Asanteni sana kwa kunisikiliza.